

OFISI YA RAISI – TAMISEMI

HALMASHAURI YA WILAYA YA RORYA.

SHULE YA SEKONDARI BUKURA
S.LP 93

SHIRATI – RORYA

10/12/2020

Kmb No. **BSS/SF/VOL 13**

MWANAFUNZI

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI BUKURA KIDATO CHA
KWANZA 2021

1.0 Nafurahi kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka 2021 katika Shule ya **Sekondari Bukura** ambayo ni ya kutwa. Shule hii ipo katika kijiji cha Bubombi, Kata ya Bukura, Tarafa ya Nyancha. Shule itafunguliwa tarehe **11/01/2021**

Mambo muhimu ya kuzingatia:-

1. SARE YA SHULE.

WAVULANA:

Suruali 2, moja NYEUSI na nyingine rangi ya KIJIVU yenye mifuko kushoto na kulia na nyuma na sio mbele. Shati mbili (2) NYEUPE (White plain) mikono mifupi, Soksi nyeusi, Viatu vyeusi vya ngozi, Mkanda mweusi/ kahawia.

Zitakaguliwa Shuleni siku atakaporipoti. **Suruali zisiwe na mshono wa modo.**

WASICHANA:

Sketi mbili (2) moja NYEUSI na nyingine rangi KIJIVU zenye urefu wa kugusa kiatu na marinda ya unene inchi mbili, Viatu vyeusi vya ngozi, Soksi nyeupe ndefu (stocking), shati mbili (2) nyeupe mikono mifupi. Zitakaguliwa Shuleni siku utakaporipoti.

Tafadhali zingatia vipimo vilivyoelekezwa hapo.

Kwa wote:

- T- shirt (fulana) rangi ya KIJIVU yenye kola ,
- Sweta rangi ya damu ya mzee.

2.0 VITENDEA KAZI:

- i. Madaftari makubwa tisa kwa ajili ya masomo ya darasani (Counter book Quire 2) ni lazima.
- ii. Bofa (Mathematical set) ni lazima
- iii. Kalamu ya wino na mkaa (pencil).
- iv. Dictionary

NB. Vifaa vyote vitakaguliwa siku mwanafunzi atakaporipoti

Kumbuka kuja na nakala ya cheti cha kuzaliwa.

Usajili utaanza tarehe **11/01/2021 – 22/01/2021**

KANUNI NA SHERIA ZA SHULE.

3.0 Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa mara baada ya kufika shuleni.

- a) Heshima kwa viongozi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii.
- b) Mahudhuri mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu
- c) Kuwahi katika shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
- d) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia maelezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- e) Kutunza usafi wa mwili na mazingira yote.
- f) Kuvaa sare ya shule wakati unapotakiwa.
- g) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
- h) kuwa msikivu na mtulivu wakati wote

4.0 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha ukafukuzwa shule.

- i. Wizi
- ii. Uasherati, ushoga na usagaji
- iii. Ubakaji
- iv. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile, uvutaji bangi, cocane, mirungu, kuberi nk
- v. Kupiga au kupigana na mwanafunzi mwenzako au mtumishi
- vi. ~~Kuharibu~~ kwa makusudi mali ya umma na ya watu wengine.
- vii. Kudharau bendera ya Taifa, wimbo wa Taifa na fedha ya Taifa.
- viii. Kuoza au kuolewa
- ix. Kupata mimba, au kuharibu mimba ndani na nje ya shule (Wasichana)
- x. Kumpa msichana mimba (Wavulana).
- xi. Kujiachisha shule mwenyewe
- xii. Kukataa adhabu halali
- xiii. Kugoma au kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa watu shuleni.
- xiv. Na makosa mengine.

5.0 TAFADHALI SOMA KWA MAKINI MAELEZO/MAAGIZO HAYA NA KUYATEKELEZA KIKAMILIFU.

KARIBU KATIKA SHULE HII

Thaula

MKUU WA SHULE

MKUU WA SHULE
BUNDA

HALMASHAUKI YA WILAYA YA RORYA

SHULE YA SEKONDARI BUKURA,
S.L.P 93,
SHIRATI-RORYA.

Kumb Na. BSS/S.F.1/VOL1/13.

Tarehe-----

MEDICAL EXAMINATION FORM (HATI YA UTHIBITISHO WA MATIBABU)

Ninathibitisha kwamba nimemchunguza mwanafunzi-----
--(Jina).

Nimemchunguza vitu vifuatavyo:-

- | 1. Kinyesi | Matokeo |
|------------------------------------|---------|
| 2. Mkojo | " |
| 3. Macho | " |
| 4. Damu (Sickle Cell B/S) | " |
| 5. Damu (Blood Pressure-BP) | " |
| 6. Kifua Kikuu (TB) | " |
| 7. Ukoma | " |
| 8. Pumu (Athma) | " |
| 9. Mimba kwa wasichana (Pregnancy) | " |
| 10. HIV (Ukimwi) | " |
| 11. Na magonjwa mengine n.k | " |

Kwa hiyo afya yake ni hafifu/timamu anastahili matibabu yafuatayo:-

- UTAONESHA HATI HII SIKU UKAPORIPOTI SHULENI.

TAREHE

SAHIHI NA MUHURI WA MGANGA MKUU HOSPITALI YA
SERIKALI